



## TANGAZO LA KAZI

Dar24 Media ni chombo cha habari cha mtandaoni kilichosajiliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), kwa mujibu wa sheria, kilichojikita katika kutoa maudhui yanayozingatia miiko na kanuni za uandishi wa habari kwa maslahi ya umma.

Tunatangaza fursa tukilenga kumpata kijana mwenye kipaji na ufanisi katika tasnia ya uandishi wa habari na utangazaji.

### **Nafasi: Mtangazaji/muandaaji wa vipindi vya habari za TV**

#### **Vigezo:**

- awe na uwezo wa kuandaa na kutangaza habari;
- awe na uwezo wa kufanya mahojiano na vyanzo mashuhuri, maarufu n.k;
- awe na uwezo wa kuandaa/kufanya makala za kijamii;
- awe na uwezo wa kuandika habari;
- awe na uwezo wa kutumia program za kompyuta zinazosaidia ufanyaji kazi za habari.
- awe mbunifu, mwaminifu, mchapakazi;
- uzoefu kuanzia miaka miwili utaongeza thamani.

#### **Kiwango cha elimu:**

- Awe amesoma uandishi wa habari kuanzia ngazi ya diploma na kuendelea, au kozi inayoendana kutoka chuo kinachokubalika na Mamlaka zinazosimamia elimu Tanzania.

#### **Majukumu Makuu:**

- kuandaa na kusoma habari, magazeti;
- kuandaa na kutangaza vipindi;
- kufanya makala;
- kufanya mahojiano na watu maarufu/mashuhuri, wateja na umma; na
- kazi nyingine zinazoendana na hizo.

#### **JINSI YA KUOMBA:**

Muombaji atume Wasifu Wake (**CV**) na **DEMO** yake (hususani ya Video), kupitia barua pepe: [dar24fursa@gmail.com](mailto:dar24fursa@gmail.com)

Demo - Unaweza kuirekodi hata kwa simu, kama hauna vifaa

#### **Mwisho wa kupokea maombi: Agosti 10, 2020**

\*Wanawake wanahimizwa kuomba zaidi

**Wasiliana nasi:** +255 679 979 786, Ofisi zetu ziko Mikocheni B, Dar es Salaam.

Imetolewa na Uongozi wa Dar24 Media.

**Agosti 3, 2020**